**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA WA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 08 Septemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 18 Juni, 2021.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Kuweka Usimamizi mzuri wa Shughuli za Kiislam Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Kuweka Usimamizi mzuri wa Shughuli za Kiislam Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

2. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Mheshimiwa Ali Abeid Karume wakati akizindua jengo la Kituo cha Afya Sizini pamoja na nyumba ya daktari mnamo tarehe 9/1/2019, aliiahidi familia ya mdau aliyejitolea kiwanja hicho marehemu Ibrahim Mzee Ali kuwa, atapewa heshima ya kuajiriwa mtoto wake mmoja ndani ya familia yake kama ahsante kwa kutoa eneo lake hilo.

Je, Serikali imeshatekeleza ahadi hiyo kwa familia ya mdau huyo muhimu.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

131. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Serikali imekuwa ikiboresha mara kwa mara sera zinazohusu maslahi ya watu wenye ulemavu. Hata hivyo, katika Jimbo la Pandani hakuonekani kujaliwa kwa haki za watu wenye ulemavu.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwatambua na kuwapa msaada kwa wakati watoto wenye ulemavu wa kutembea ambao wanahitaji kwenda skuli na vyuoni.

(b) Je, Serikali ina jukumu gani la kuwatunza na kuwawezesha wazee waliokatwa miguu yao kwa ugonjwa au kwa ajali na ambao hawajiwezi.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

14. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa nia njema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuanzisha Mahkama ya Kupambana na Kukabiliana na Vitendo vya Udhalilishaji.

(a) Kwa kuwa uamuzi huo umeamuliwa tangu mwanzo wa mwaka 2020. Je, Mahkama hizo zipo maeneo gani ya Unguja na Pemba.

(b) Katika utekelezaji wa agizo hilo, Je, Serikali imewateuwa Mahakimu wangapi kwa Unguja na wangapi kwa Pemba kwa ajili ya kufanikisha lengo hilo la Serikali.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

19. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa Kojani ni kisiwa kilichopewa hadhi ya kuwa Wilaya ndogo, na kwa kuwa hapo zamani kisiwa hicho kilikuwa na Wadi inayojitegemea, na kwa kuwa hivi sasa Wadi ya Kojani imechanganywa na vijiji vilivyoko nje ya kisiwa hicho jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa kwa Diwani wa Wadi hiyo pamoja na kupunguza nguvu za maendeleo kwa wakaazi wa kisiwa cha Kojani ambao idadi yao inaongezeka maradufu siku hadi siku.

Je, ni lini Serikali itakirudishia kisiwa cha Kojani Wadi yake inayojitegemea bila ya kushirikiana na vijiji vilivyomo nje ya kisiwa hicho.

**Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:**

9. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na changamoto ya ukosefu wa vifaa vya michezo kwa watu wenye ulemavu, jambo ambalo huwafanya kushindwa kushiriki katika michezo ya kitaifa na kimataifa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vifaa ili waweze kushiriki mashindano mbali mbali na kuinua vipaji vyao.

122. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kufuatia agizo la Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) la kuendeleza mazoezi, siku ya Jumamosi ya tarehe 07-08-2021, wakati akiwahutubia washiriki wa mazoezi ya vijana wa CCM (UVCCM), Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo aliahidi mbele ya vyombo vya Habari kwamba, Jumamosi ya mwanzo wa kila mwezi, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo itadhamini mazoezi hayo.

(a) Je, udhamini huu wa Serikali ni kwa ajili ya mazoezi ya vijana wa CCM (UVCCM) peke yao au kuna fursa kwa vijana wa vyama vingine kudhaminiwa.

(b) Je, ni programu ipi katika bajeti ya 2021/2022 imepangwa kutoa udhamini huo.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuepuka kudhamini aina hii ya huduma ili kuondoa dhana ya mgongano wa maslahi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

7. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Miongoni mwa changamoto inazozikabili Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) ni pamoja na kuwepo kwa ongezeko la madeni kwa taasisi za Serikali, hali inayolipelekea kupunguza mapato yake.

(a) Je, kuna kikwazo gani kwa taasisi za Serikali kushindwa kulipa madeni yao kwa ZECO licha ya taasisi hizo kupitishiwa bajeti zao kila mwaka.

(b) Je, Serikali italisaidia vipi Shirika hili ili madeni wanayoyadai kwa taasisi mbali mbali za Serikali yaweze kulipwa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

97. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wazanzibari walio wengi wanajishughulisha na suala la kilimo kama utamaduni wao ili kujipatia riziki. Kwa sasa mazao mengi wanayolima hayana tija kubwa kutokana na miundombinu dhaifu ya kilimo, hivyo kushindwa kuzalisha kwa kiwango kinachokusudiwa.

a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia wakulima wetu hawa mbegu bora na za kisasa ili ziweze kuwapatia kipato zaidi na familia zao.

b) Je, Wizara yako imejipanga vipi katika kuboresha miundombinu ya kilimo kwa wakulima wetu ili kuondokana na utegemezi wa chakula kutoka nje ya Zanzibar.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

53. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Miongoni mwa chanzo cha mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni utoaji wa leseni za udereva na njia. Kazi hiyo inatekelezwa kupitia Mamlaka ya Usafiri na Leseni iliyopo Mwanakwerekwe Zanzibar.

(a) Je, kwanini wananchi wanasumbuka sana wanapokwenda kupata huduma hizo kwa kutumia muda mkubwa pasi na kuwepo ulazimu huo.

(b) Kwanini muda mwingi madirisha yanayotoa huduma huwa hayana wafanyakazi na kusababisha foleni kubwa katika madirisha machache.

(c) Kwanini kusikuwepo dirisha maalum litakaloshughulikia wateja wanaorudi kufanya malipo ya huduma wanayohitaji ili kuepusha kuanza upya kupanga foleni.

62. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kuna Kampuni za uwakala zinazoandikisha mabaharia kwa ajili ya kazi katika meli za nje mfano KONAIKA.

(a) Je, Kampuni hizo zimesajiliwa kwa mujibu wa sheria zetu.

(b) Je, zinapotokea ajali au vifo baharia wanapatiwa stahiki zao kwa mujibu wa sheria.

(c) Je, viwango wanavyolipwa vinatolewa kwa vigezo gani.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

75. MHESHIMIWA HABIB ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo na Amali:

Mheshimiwa Waziri ni kawaida kwa mradi wa maendeleo kuwa na malengo yanayotakiwa kufikiwa baada ya utekelezaji. Hivyo, basi tunaomba kujua

(a) Ni kwa kiasi gani mradi wa ZISP umefikia malengo tarajiwa.

(b) Ni maeneo yepi ambayo tunaweza kuthibitisha katika skuli mbali mbali kuhusiana na mafanikio ya mradi huu nchini Zanzibar.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

36. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Imebainika kuwa, kuna baadhi ya wagonjwa katika hospitali zetu kisiwani Pemba hutakiwa kulipia gharama za safari kwa daktari anayeambatana nae pale anapopata uhamisho wa kimatibabu katika hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara yako inalifahamu suala hili.

(b) Na kama inalifahamu, Je, ni sahihi kwa madaktari hao kufanya kitendo hicho.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

3. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Licha ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchukua jitihada kubwa ya kuwaletea neema wananchi wake kuhusu kilimo cha mwani, bado kuna changamoto nyingi zinazorejesha nyuma kipato cha mkulima, ikiwemo bei ndogo pamoja na matajiri kuchelewesha kununua na kuwaacha wananchi kubakia na mwani muda usiojulikana.

(a) Je, ni lini suala la bei ya mwani litapatiwa ufumbuzi ili wananchi wetu waendelee kufurahia shughuli wanazozifanya.

(b) Je, kuna mkakati gani wa kampuni zinazonunua mwani, kununua bidhaa hiyo kwa wakati.

(c) Je, ni Wilaya ipi katika kisiwa cha Pemba inayoongoza kwa uzalishaji wa mwani.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

70. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika Uchumi wa Buluu shughuli nyingi sana zitafanywa katika maeneo ya bahari ikiwemo uchimbaji wa mafuta, madini, ufugaji wa samaki na uvuvi. Kila moja katika shughuli hizo itadai nafasi yake.

(a) Je, Zanzibar imeshaandaa mipango ya mazingira ya habari “M.S.P” (Marine Special Planning).

(b) Je, Zanzibar imejipangaje katika usimamizi wa mazingira ya bahari.

(c) Je, utafiti juu ya mipango ya mazingira ya baharini (Marine Special Planning) umefanyika Zanzibar.

## IV. <u>HOJA ZA SERIKALI</u>

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Kuweka Usimamizi mzuri wa Shughuli za Kiislam Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**08 Septemba, 2021.** **<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**